
# Habari za Manmin

NA. 772 MACHI 9, 2025

Watu Walio Kutana na Mungu


## "Nilipona Malengelenge Makali!"

Ndugu Dooyoung Cho | 55, Bang-yi Dong, Songpa Gu, Seoul, Korea

Mnamo Desemba 2024, nilihisi muwasho kwenye kwapa langu la kulia na mgongo. Nilidhani ni ugonjwa wa ngozi, lakini malengelenge na maumivu makali yakaanza. Hata kuguswa na nguo kulisababisha maumivu makali, nikapata ugumu kuendelea na shughuli za kila siku.

Nilipoenda hospitalini, nilipatikana na malengelenge. Daktari alisema ingekuwa bora ningekuja mapema na akanipa dawa, akiahidi kuzibadilisha kulingana na hali yangu.

Nilianza kutumia dawa, lakini maumivu yaliendelea, hivyo nikaacha. Katika maombi, nilitafakari maisha yangu na kugundua makosa yangu katika maneno na matendo...makosa katika kutekeleza majukumu yangu niliyopewa na Mungu, na nikatubu.

Kabla ya kupata malengelenge,





Kabla ya maombi



Baada ya maombi

nilihisi mzigo mzito katika kutimiza wajibu wangu kutokana na mawazo yangu ya kimwili. Oktoba iliyopita, nilizungumza na mchungaji mlezi nikihisi mzigo kuhusu majukumu yangu. Lakini nilipotubu, nilitambua kwa kina kwamba sipaswi kuyatekeleza kwa nguvu na uwezo wangu mwenyewe, bali kwa uweza wa Mungu Baba, ambaye hutimiza ufalme wake mwenyewe.

Tangu wakati huo, moyo wangu ulijawa na furaha na amani, nikihisi urejesho wa upendo wangu wa kwanza kwa Bwana. Nilianza kunyunyiza maji matamu ya Muan kwenye sehemu zilizoathirika mara moja kwa siku. Wakati wa ibada za Jumapili na mikutano ya maombi ya Danieli, nilipokea maombi ya Mchungaji Mkuu Soojin Lee kwa imani, nikiamini kuwa Mungu ataniponya.

Kwa mshangao wangu, maumivu yaliyodumu kwa wiki 3 au 4 yalitoweka kabisa, na nikapona kikamilifu! Haleluya! Sasa sijihisi tena mzigo juu ya majukumu yangu bali nayakabidhi mikononi mwa Mungu, na kwa neema yake, amenipa majukumu mengi zaidi. Kupitia uponyaji huu, Mungu ameimarisha imani yangu, na nimeshuhudia upendo wake mkuu. Nitaendelea kusonga mbele kwa bidii, nikilenga kulipa neema yake kwa maisha yangu yote.

# "Vivimbe vyangu vya mapafu ambavyo vilionekana vingeendelea kuwa saratani vilitoweka"

Dada Boknam Jang | Miaka 57, Sangdo-dong, Dongjak-gu, Seoul, Korea




Mnamo Novemba 18, 2023, nilihisi maumivu makali kifuani kwangu upande wa kulia, na kila nilipopumua, nilihisi kana kwamba nimechomwa kwa kisu. Sikuweza kukaa, kusimama, wala kulala sakafuni. Nilihisi kuwa sikuwahi kupata maumivu makali kama hayo, na nikatafakari maisha yangu ya nyuma. Kwanza, nilitubu kwa kuwaumiza wengine kwa maneno yangu. Lakini maumivu yangu hayakupungua, bali yalizidi kuwa mabaya zaidi. Nilihisi kama ningekufa, na mnamo Novemba 21, nilienda kwenye kliniki ya mji wangu. Uchunguzi ulionyesha kuwa joto la mwili wangu lilikuwa nyuzi 38, na niligunduliwa kuwa na kuchomwa na asidi ya mwili kooni. Daktari alinipa dawa, lakini sikuitumia. Niliteseka kwa homa kali kwa siku chache zilizofuata na kuvumilia maumivu makali sana. Nilikuwa na makohozi mazito ya manjano. Kwa kuwa niliogopa kwamba koo langu lingeumia zaidi nikiyameza, niliyatoa kwa kukohoa mfululizo.

Mnamo Novemba 29, 2023, nilihudhuria Mkutano wa Uponyaji wa Kiungu na kwa bidii nikapokea maombi kutoka kwa Mchungaji Soojin Lee kwa ajili ya wagonjwa. Baada ya hapo, maumivu yangu yalizidi kupungua. Siku chache baadaye, nilienda hospitalini kwa uchunguzi zaidi wa ugonjwa wangu. Nilipatikana kuwa na nimonia, na daktari alinipa dawa za kunywa kwa wiki tatu. Sikuchukua dawa hizo. Daktari wangu alisema kuwa kulikuwa na uvimbe kwenye mshipa wa damu wa kifua changu cha kulia na akanishauri niende kwenye kituo kikubwa cha saratani. Nilipoenda kwenye kituo cha saratani na kufanyiwa uchunguzi, daktari aliniambia, "Umepona nimonia kwa sababu ulitumia dawa vizuri." Lakini nikamjibu, "Sikunywa dawa hata kidogo." Akaniuliza kwa ukali, "Mbona umekuja hapa ikiwa hukufuata maagizo ya matibabu?" Akanipa dawa tena na kunionya kuwa ni lazima nizitumie. Lakini nikakumbuka kuwa niliwahi kuponywa uvimbe kutokana na kifua kikuu kupitia maombi ya Mchungaji Mkuu Soojin Lee, hivyo sikutumia dawa hata wakati huu pia.

Niliporudia matokeo, daktari aliniambia nilazwe kwa uchunguzi wa kina zaidi, pamoja na uchunguzi wa tishu. Lakini nilikataa kulazwa hospitalini, bali niliondoka. Siku iliyofuata, nilipokea simu kutoka kituo cha saratani, na matokeo yalionyesha kuwa uvimbe ulipungua na hapakuwa na haja ya kufanya uchunguzi wa tishu. Muuguzi alisema kuwa dawa yao ilikuwa imenisaidia na akanishauri nitumie dawa hizo kwa wiki tatu. Lakini kwa kweli, sijawahi kunywa dawa kwa mwaka mmoja uliopita, lakini nimekuwa na afya njema bila maumivu yoyote. Namshukuru na kumpa utukufu Mungu aliyeniponya.

**Maelezo ya daktari**




Kabla ya Maombi: Ondoa uwezekano wa saratani ya mapafu


**"Mchungaji Soojin Lee – 'Biblia Pekee'"**

ni kipindi cha YouTube chenye lugha mbalimbali.

Inakuleta barua ya upendo wa Mungu, Iliyofichwa katika Maandiko,
Na upendo wa Bwana Unaomiminika kwa wingi.




Imewekewa manukuu kwa lugha 13 kama vile Kiingereza, Kichina, Kijapani, Kihispania, Kirusi, Kifaransa, Kiurdu, Kihindi, Kiswahili, Kitamil, Kiromania, na Kiebrania.


** Unaweza kutazama 'Biblia Pekee' kwa kuskani msimbo wa QR.

# "Niliponywa kutokana na kuvunjika mfupa wa goti nikiwa katika hatari ya upasuaji!"


"Dada Changsoon Won | Miaka 70, Dogsan Dong, Geumcheon Gu, Seoul, Korea."



Matokeo ya X-ray



Kabla ya maombi: Kuvunjika kwa patela pamoja na uso wa pamoja.



Baada ya maombi: Muunganiko wa mfupa umekamilika.

Mnamo Oktoba 13, 2024, nilikuwa kwenye kivuko cha watembeaji, na taa ya trafiki ilipokuwa inabadilika kuwa nyekundu, niliharakisha kukimbia lakini nikateleza. Baada ya kuanguka, goti langu la kushoto liliniuma sana, na ilikuwa vigumu kwangu kutembea vizuri. Kwa msaada wa watu waliokuwa karibu nami, nilifanikiwa kurudi nyumbani kwa shida.

Asubuhi ya siku iliyofuata, nilimpigia simu mchungaji wangu mkuu mpendwa, Geumran Hwang, naye akaniombea kwa simu. Baada ya maombi hayo, maumivu yalipungua, na nilienda hospitalini kwa uchunguzi. Kupitia matokeo ya X-ray, daktari aliniambia, "Umevunjika mfupa wa goti la kushoto, unahitaji upasuaji." Lakini sikufanyiwa upasuaji, badala yake nilirudi nyumbani nikiwa nimevaa kifujo cha plastiki.

Nilifikiria kwa kina ni kwa nini jambo hili lilinitokea na nikatafakari kuhusu maisha yangu ya nyuma. Nilitubu kwa sababu ya hasira yangu ya haraka, hisia mbaya, wivu, kuhukumu, kulaumu, na kwa kutokuwa na bidii katika maombi.

Baadaye, kila nilipohudhuria ibada za asubuhi za Jumapili, nilipokea maombi ya Mchungaji Mkuu Soojin Lee kwa ajili ya wagonjwa. Mnamo Oktoba 29, Parokia za Kichina 2 & 3 ziliandaa mkutano maalum wa maombi kwa ajili ya ujazo wa Roho Mtakatifu, na kwa msaada wa mume wangu na kiongozi wa wilaya yangu, nilichukua teksi kwenda kuhudhuria.

Mhubiri Mchungaji Miyoung Lee aliniombea, na moto wa Roho Mtakatifu ukanijia. Nilihisi kana kwamba kichwa changu, kiuno, na miguu yangu ilikuwa moto na yenye uhai mpya. Njiani kurudi nyumbani baada ya mkutano, sikuwa na maumivu tena, na niliweza kukanyaga chini kwa mguu wangu wa kushoto!

Nilitamani kupona kabisa, hivyo nikachunguza maisha yangu kwa kusoma kitabu cha "Ujumbe wa Msalaba." Nilitubu kwa makosa yangu ya kina, kama vile kutotimiza majukumu yangu kwa dhati.

Mnamo Novemba 1, nilihudhuria ibada ya usiku ya Ijumaa kwa furaha, kisha nikaota ndoto kuhusu Mchungaji Mkuu Soojin Lee. Katika ndoto hiyo, aliniambia, "Simama utembee!" Nilipoamka, nilihisi uhakika wa uponyaji wangu. Baadaye, niliondoa kifujo cha plastiki na kujaribu kusogeza mguu wangu—niliweza kutembea vizuri bila fimbo niliyokuwa nikiitegemea. Halleluya!

Zaidi ya hayo, nilikuwa nikihisi uvimbe wa ukubwa wa nyanya ndogo upande wa kushoto wa shingo yangu kwa miaka miwili. Asubuhi moja nilipoamka, niligundua kuwa ulikuwa umetoweka kabisa!

Nilitaka kuthibitisha kiafya, hivyo nilienda hospitalini kwa uchunguzi wa kimatibabu mnamo Novemba 14. Daktari alisema, "Mgonjwa mwenye kuvunjika kwa mfupa wa goti hawezi kusogeza mguu wake hata baada ya mwezi mmoja. Ni muujiza kwamba unaweza kuusogeza ndani ya wiki tatu tu bila upasuaji!" Kisha akaongeza, "Kuvunjika kwako kumepona kabisa!" Halleluya!

Natoa shukrani na utukufu kwa Mungu Baba aliyeniponya kutokana na kuvunjika kwa mfupa wa goti bila upasuaji.



## Mkutano wa Uponyaji wa Kiungu

Fursa maalum kwa afya na furaha yako!
Miujiza ya uponyaji na majibu tele
kupitia kazi ya moto wa Roho Mtakatifu!
Njoo uone muujiza mpya na maisha mapya!

"Saa 5:00 usiku, Ijumaa, Machi 28, 2025
Katika Kanisa Kuu la Manmin
Na Mchungaji Mkuu Soojin Lee"

Inapeperushwa moja kwa moja kwenye GCN TV! (www.gcntv.org)



# Kwa nini Yesu, Mwana wa Mungu, alivaa taji la miiba?

Aliposhuka duniani kuja kuwaokoa wanadamu kutoka kwa dhambi, Yesu alilazimika kuvaa taji la miiba. Kwa nini alifanya hivyo?

### 1. Sababu ya Yesu kuvaa taji la miiba kichwani na kutoka damu.

Sababu ambayo Yesu alilazimika kuvaa taji la miiba na kumwaga damu yake isiyo na hatia ni kutukomboa kutoka kwa dhambi tulizotenda katika mawazo yetu.

Tuna mfumo wa kumbukumbu katika ubongo wetu unaohifadhi maarifa. Tangu kuzaliwa, kile tunachojifunza huhifadhiwa kwenye mfumo huu wa kumbukumbu pamoja na hisia zetu, kinachoitwa 'maarifa.' Kila mtu ana malezi na elimu tofauti, na kwa mafundisho yale yale, kila mmoja huwa na maadili na vigezo tofauti vya kutofautisha mema na mabaya kulingana na jinsi alivyojifunza.

Maarifa yaliyohifadhiwa katika ubongo yanaporejeshwa katika kumbukumbu, huitwa 'mawazo.' Kwa kuwa watu wana maarifa tofauti, kwa tukio lile lile, wengine huliona kuwa jema ilhali wengine huliona kuwa baya. Shetani hudhibiti mawazo ya wanadamu wenye dhambi, na mara nyingi mawazo yao huwa kinyume na kweli.

Kwa hiyo, tunapaswa kusikiliza Neno kwa bidii, kulifanya kuwa chakula chetu cha kiroho, na kulitenda kwa kusema "Ndiyo" na "Amina" ili tubadilishwe kwa kufanywa upya katika mawazo yetu.

### 2. Jinsi ya kuacha mawazo ya kimwili na kuwa na mawazo ya kiroho.

> "Wale askari wakampeleka ndani ya jumba la kifalme (yaani, Praetorium), wakakusanya kikosi chote cha Warumi. Wakampandisha vazi la rangi ya zambarau, kisha wakasokota taji la miiba na kumvika." (Marko 15:16-17)

Unaposikiliza Neno la Mungu, unaweza kusema 'Amina' kwa yale yanayolingana na mawazo yako na kuyaamini. Lakini yale yasiyolingana na maarifa na uzoefu wako huenda usiyaamini. Hii inaweza kukuingiza katika mawazo yanayopingana na mapenzi ya Mungu, yanayoitwa 'mawazo ya kimwili' (Warumi 8:7).

Tunapaswa kuharibu mawazo ya kimwili yanayotuzuia kuamini Neno la Mungu na kulitii. Lazima tuvunje hoja zote na kila kitu kinachojiinua kinyume na maarifa ya Mungu, na kufanya kila fikra kuwa mateka kwa utiifu wa Kristo (2 Wakorintho 10:5).

Je, tunapaswa kufanya nini ili kuondoa dhambi hii katika mawazo yetu? Tunapaswa kutakasa mioyo yetu, kwa kuwa uovu ndani ya moyo huleta mawazo ya kimwili.

Tamaa ya mwili hutufanya tutafute mambo ya ulimwengu, na tamaa hii ikiongezeka, husababisha matendo ya mwili (Wagalatia 5:19-21). Tamaa ya macho huchochea mawazo yetu kupitia kile tunachoona na kusikia, na hutufanya tutamani mambo ya kidunia.

Kiburi cha maisha hutufanya tutafute anasa za dunia na kutaka kuonekana bora kwa wengine. Kwa sababu ya kiburi hiki, tunataka kuheshimiwa, kusifiwa, na kupata mamlaka zaidi. Hatutaweza kutakasa mioyo yetu kikamilifu hadi tuondoe tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha maisha. Ni hapo tu ndipo tutakapokuwa na mawazo ya kiroho yanayompendeza Mungu.

### 3. Mungu anatutayarishia taji nzuri mbinguni

Yesu alipovaa taji la miiba na kumwaga damu, alifungua mlango wa msamaha kwa dhambi za mawazo yetu na kutuandalia taji nzuri mbinguni.

Mbinguni kuna taji tofauti kulingana na jinsi tulivyoishi duniani. Taji isiyoharibika hutolewa kwa wale waliompokea Bwana na kupambana na dhambi (1 Wakorintho 9:25). Taji ya utukufu hupewa wale waliotii Neno la Mungu na kumtukuza (1 Petro 5). Taji ya uzima hutolewa kwa wale waliotakaswa kwa kuondoa uovu wote na kubaki waaminifu hadi mwisho kwa upendo wa Mungu (Yakobo 1:12; Ufunuo 2:10).

Taji ya haki na taji ya dhahabu hutolewa kwa wale waliotakaswa kikamilifu na kutimiza wajibu wao kwa imani inayompendeza Mungu (2 Timotheo 4:8; Ufunuo 4:4). Mungu wetu mwenye upendo atatupa taji kulingana na kiwango cha utakatifu na uaminifu wetu.

< Itaendelea......

Swahili
Habari Za Manmin
Imechapishwa na Kanisa Kuu la Manmin.
Mchapishaji: Soojin Lee | Mhariri: Johnny Kim | Imetafsiriwa na Ofisi ya GCN Nairobi.
73 Yeoidaebang-Ro 22-Gil, Dongjak-Gu, Seoul, Korea
(Nambari ya Posta: 07056)
http://www.manmin.org/english
www.manminnews.com
Barua Pepe : manminhq@manmin.kr